

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Simu: +255-26-2323189
Barua pepe: ps@moha.go.tz
Tovuti: www.moha.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Habari/Afya,
S.L.P. 2916,
40483 DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

**UHAKIKI WA TAASISI ZA KIDINI NA JUMUIYA ZA KIJAMII
KATIKA KANDA YA MAGHARIBI KUFANYIKA KUANZIA
TAREHE 6 JUNI HADI TAREHE 16 JUNI 2021**

4 Juni, 2021

1. Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) zinatarajia kuendesha zoezi la uhakiki wa Taasisi za Kidini, Jumuiya mbalimbali za kijamii na Bodi za Wadhamini katika Kanda ya Magharibi. Zoezi hilo litafanyika kuanzia tarehe 6 Juni, 2021 hadi 16 Juni, 2021 likihusisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi. Kituo cha uhakiki kitakuwa katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Tabora kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.
2. Malipo ya ada yatafanyika wakati wa Zoezi la Uhakiki kupitia Mfumo wa Malipo wa Serikali kwa njia ya Kieletroniki (Government Electronic Payment Gateway System).
3. Kadhalika, wananchi wote wanajulishwa kuwa wakati wa Zoezi la Uhakiki nyaraka zifuatazo zinatakiwa kuwasilishwa; -
 - i. Cheti Halisi cha Usajili wa Jumuiya na Bodi ya Wadhamini pamoja na Kivuli cha Vyeti hivyo.
 - ii. Stakabadhi za malipo ya ada kwa miaka ya nyuma pamoja na kivuli cha fomu ya marejesho ya Wadhamini kwa upande wa Bodi za Wadhamini.
 - iii. Katiba na Kanuni za Jumuiya/Taasisi/Bodi ya Wadhamini husika zilizopitishwa na Msajili au Mtendaji Mkuu wa RITA pamoja na vivuli vya nyaraka hizo.
 - iv. Barua inayothibitisha uwepo wa Jumuiya/Taasisi/Bodi ya Wadhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kata wa mahali ilipo Ofisi ya Jumuiya/Taasisi/Bodi ya Wadhamini wa Taasisi husika.
 - v. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka na Taarifa ya Fedha ya Mwaka.
 - vi. Fomu za Uhakiki kwa Jumuiya zilizosajiliwa katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ni www.moha.go.tz, Kwa upande wa Bodi za Wadhamini Fomu zinapatikana kwenye tovuti ya Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) ambayo ni www.rita.go.tz pamoja na kwenye Kituo cha Uhakiki.
4. Taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa katika zoezi hili zitalazimika kwenda kuhakikiwa katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii iliyopo Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 11 Jijini Dodoma na katika Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) iliyopo Jengo la RITA, Posta, Jijini Dar es salaam.
5. Huduma ya usajili kwa Jumuiya za Kidini na Zisizo za Kidini pamoja na Bodi za Wadhamini zitatolewa katika Kituo cha Uhakiki. Hivyo, Viongozi wa Taasisi na Vikundi mbalimbali vyenye sifa ya kusajiliwa kuwa Jumuiya, wanahimizwa kujitokeza ili waweze kupatiwa utaratibu wa kusajili Taasisi na Vikundi vyao.
6. Sambamba na zoezi hilo la Uhakiki, Elimu kwa Umma juu ya aina ya vyama, vikundi na taasisi zinazopaswa kusajiliwa katika Ofisi hizo mbili itatolewa pamoja na elimu juu ya maana na uhusiano uliopo kati ya Taasisi zinazosajiliwa katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya na Bodi za Wadhamini zinazosajiliwa RITA.

Imetolewa na:

MSAJILI WA JUMUIYA ZA KIJAMII